



**TAARIFA KWA UMMA
MAOMBI YA LESENI ZA NJIA MAALUM ZA DALADALA KWA
KAMPUNI AU USHIRIKA - DAR ES SALAAM**

Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) kwa kushirikiana na wadau wa usafirishaji inaendelea na mkakati wa kuboresha huduma za usafiri mkoani Dar es Salaam. Katika mkakati huo, Mamlaka imetenga njia maalum zitakazohudumiwa na wasafirishaji wenyе magari ambayo yana umiliki wa Kampuni, Vyama au Ushirika.

Hivyo, Mamlaka inawakaribisha wasafirishaji wote wenyе magari kuanzia kumi (10) na kuendelea, wenyе kampuni, waliopo kwenye vyama au ushirika kufika katika ofisi za LATRA Mkoa wa Dar es Salaam ili kupata utaratibu wa kushiriki kwenye mkakati huu.

Imetolewa na:

Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano
06 Aprili, 2023